**Joseph Ngussa Bohole, (1938–2009)**

Joseph Ngussa Bohole alikuwa mchungaji na mwinjilisti mashuhuri wa vitabu ambaye alijitolea kuchukua jukumu muhimu katika kuleta roho nyingi kwa Kristo kote nchini Tanzania.

**Maisha ya Awali, Elimu, na Ndoa**

Joseph Ngussa Bohole alikuwa mtoto wa Kihoja Bohole na Misana Noni ambao walikuwa waumini wa dini ya jadi ya Kiafrika ya kuabudu mizimu. Alizaliwa Januari 1, 1938, huko Itilima katika Mkoa wa Simiyu, nchini Tanzania. Bohole hakupata elimu rasmi kwani familia yake ilimhitaji kufanya kazi nao katika maisha yao ya kilimo na ufugaji. Lakini kutokana na dhamira yake ya kupenda elimu, Bohole alijifunza kusoma na kuandika chini ya malezi ya rafiki yake, Daniel Sayi, ambaye alikaa naye chini ya mti kwenye kijiji cha Ng'wanunui ili kujifunza. Huyu huyu Daniel Sayi ndiye pia aliyeitambulisha imani ya Waadventista kwa mara ya kwanza kwa Bohole. Ingawa hakupokea hati yoyote ya kitaaluma, uwezo wake wa kusoma na kuandika ulifanana na mtu aliyekuwa amemaliza darasa la nane la wakati huo. Uwezo wake kielimu unadhihirishwa na ukweli kuwa Bohole aliweza kusoma vitabu vya Roho ya Unabii, ambavyo katika siku hizo vilikuwa katika lugha ya Kiingereza pekee. Bohole alimwoa Bathsheba Masele Katema, mmoja wa waongofu wa kwanza katika Mkoa wa Tabora nchini Tanzania mnamo Septemba 1966. Bohole na mkewe walibahatika kupata watoto saba, Jacob, Emmanuel, Steven, Esther, Baraka, Furaha, na Amani.

**Uchungaji**

Kufuatia tukio la uinjilisti wa hadhara lililofanywa katika kijiji cha Ng'wanunui ukiendeshwa na mwinjilisti Haruni Kija Mashigani, Bohole aliamua kubatizwa mwaka 1958. Mara baada ya kubatizwa alianza uinjilisti wa vitabu katika mkoa wa Shinyanga, na mwaka 1964 alitumwa Tabora kama mmoja wa wanatimu katika kampeni ya mikutano ya hadhara iliyofanywa na Gabriel Mbwana ambapo Peter Katema na dada yake Bathsheba (ambaye baadaye alikuja kuwa mke wa Bohole) walibatizwa na Haruni Kija Mashigani. Hawa walikuwa waongofu wa kwanza katika eneo hilo. Katika mwaka huo huo, Bohole alihudhuria semina ya uinjilisti wa vitabu huko Busegwe, yaliyokuwa makao makuu ya Union ya Tanzania wakati huo ambapo alipata mafunzo ya kina kuhusu uinjilisti wa vitabu na uongozi kutoka kwa Ruddy Hening, aliyekuwa mkurugenzi wa uchapishaji wa Union ya Tanzania ya wakati huo.

Mnamo 1965, Bohole alihudhuria semina ya uinjilisti wa vitabu katika Shule ya Kati ya Bupandagila. Muda mfupi baada ya semina hii, alitumwa Kahama kufanya kazi na mwenzake aitwaye Mika Kamambi. Kuanzia 1966 hadi 1970, Bohole alikua mwinjilisti wa vitabu mwenye mafanikio, akifanya kazi huko Wenya - Itubilo, Mkoa wa Simiyu, na Mwanza. Kuanzia 1969 hadi 1970, alihudumu kama mchungaji katika Wilaya ya Wenya. Alitumwa kufanya kazi ya mwinjilisti wa vitabu katika eneo lisiloweza kufikiwa huko Bukoba, Kagera, akifanya kazi na mwenzake Daudi Balula kuanzia 1970 hadi

1974. Juhudi zao zilileta roho nyingi kwa Yesu Kristo kupitia vitabu. Kuanzia 1974 hadi 1982, Bohole alifanya kazi kama mkurugenzi msaidizi wa idara ya uchapishaji katika kanda ya Shinyanga na Sengerema, ambako alifundisha wainjilisti wengi wa vitabu waliofaulu, ambao baadhi yao baadaye wakawa wahudumu wa injili au wachungaji. Alifanya kazi kwa muda mfupi kama mchungaji kwa mara nyingine tena, kati ya 1982 na 1984, huko Magu, Wilaya ya Usimau. Kwa muda uliosalia wa uchungaji wake, kuanzia 1984 hadi alipostaafu mwaka 2003, alihudumu kama mkurugenzi msaidizi wa idara ya uchapishaji katika kanda za Sengerema na Bariadi. Katika kipindi hiki, pia alitumia muda wake kama mwinjilisti wa umma aliyefanikiwa na mwalimu wa Biblia kote nchini Tanzania. Kwa mfano, Mei 1990 mwenyekiti wa Union ya Tanzania, Robert Taylor, alitoa Biblia 1,500 na seti 1,500 za masomo ya Biblia huko Shinyanga wakati wa mfululizo wa mkutano wa uinjilisti uliotolewa na Zakayo Kusekwa. Chini ya uongozi wa Joseph Bohole, watu 2,121 walihusika katika kujifunza Biblia. Nusu ya hawa walibatizwa na kazi ya kuwakatisha shauri wale waliokuwa bado hawajafanya maamuzi ya ubatizo iliendelea. Matukio kama haya yalifanyika Kahama, Mbeya, Tarime na Bariadi ambapo maelfu ya roho zililetwa kwa Kristo kupitia kazi ya Bohole

Bathsheba mke wa Bohole (1940-2020) alikuwa mpishi bora. Alitayarisha chakula bora kwa ajili ya familia yake na kuwafundisha wanawake wengine kufanya vivyo hivyo kwa familia zao. Alikuwa mwinjilisti mashuhuri wa vitabu aliyependa kazi yake, na kupitia mvuto wake watoto wake wakawa wanafunzi wauzao vitabu kwa ajili ya kujipatia ada ya shule wenye mafanikio katika Tanzania, Kenya, Uganda, Botswana, na Norway. Akiwa na mume wake, aliwafundisha watoto wake kumpenda Bwana na kulitumikia kanisa lake popote pale Bwana atakapowaita. Aliwahimiza watoto wake wawe na roho ya umishionari akisema, “wakati wowote, wakati wowote Bwana anapokuita kumfanyia kazi ya mbali au karibu, usisite. Pokea kwa furaha wito wa kazi ya Mungu.”

Kulingana na mafundisho ya Biblia kuhusu elimu, Bohole na mkewe waliishi maisha rahisi ya kujitoa ili kuhakikisha kwamba watoto wao wanapata elimu ya juu zaidi iwezekanavyo katika shule za Waadventista, vyuo vya kati na vyuo vikuu. Walikuwa wakiwaambia watoto wao kuwa, “elimu ni uwekezaji bora maishani. Kwa hivyo, soma kwa bidii na uwe tayari kumtumikia Bwana katika shamba lake la mizabibu.” Waliwafundisha watoto wao kufunga na kuomba kwa ajili ya changamoto ambazo mwanafamilia yeyote anakumbana nazo, jambo ambalo linaendelea katika familia za watoto wao hadi sasa. Waliwalea watoto wao kwa uaminifu katika kumcha Bwana.

Kando na huduma yake kwa kanisa, Joseph na Bathsheba Bohole waliifanya nyumba yao kuwa kama kanisa ambapo watoto wao walipewa nyadhifa za uongozi kila mwaka kupitia uchaguzi. Kwa njia hii, waliwafunza watoto wao kuwa wazee, mashemasi, wakurugenzi wa uwakili, na wasimamizi wa Shule ya Sabato. Inaelekea kuwa mazoea haya yaliboresha na kuwatayarisha watoto wao kwa uchungaji. Moja ya mchango wao wa kipekee kwa kanisa la Tanzania ni kwamba wana wao wanne kati ya watano

walitumikia Kanisa la Waadventista Wasabato katika huduma mbalimbali. Binti zao wawili wakawa Waadventista waaminifu ambao walimtumikia Bwana katika makanisa yao ya mtaa kwa njia ya uimbaji na majukumu mengine ya kanisa. Nafasi za uongozi wa kanisa zilizowahi kushikiliwa na watoto wao ni pamoja na mwenyekiti wa konferensi, mkurugenzi wa idara ya Union na konferensi, mlezi wa kiroho wa taasisi, na profesa msaidizi katika Chuo Kikuu cha Arusha nchini Tanzania.

Joseph Ngussa Bohole alifariki mnamo Mei 15, 2009, na mkewe alifariki mnamo Januari 3, 2020, wakiacha watoto saba na wajukuu kumi na wawili. Mmoja wa viongozi wa zamani wa makanisa nchini Tanzania alimuelezea Joseph Ngussa Bohole kama "mwalimu wa Biblia mwenye nguvu katika mikutano ya kambi. Alifanya kazi nzuri sana katika kufuatilia kazi baada ya uinjilisti wa umma kote Tanzania."